

# Vidokezo vya Likizo Yenye Usalama Dhidi ya COVID-19

Kadiri **watu wengi** kutoka familia tofauti mtu anashirikiana nao kwenye mkusanyiko, ndivyo mwingiliano wa **karibu** wa mwili, na **kadri mwingiliano unadumu**, ndivyo hatari **inaongezeka** ya mtu aliye na COVID-19 kueneza kwa wengine, iwe yeye ana dalili au la.

Mkusanyiko salama kabisa wa likizo ni pamoja na wale wanaoishi nyumbani kwako. Ikiwa utachagua kuwa na mkusanyiko, fikiria jinsi unaweza kupunguza kuenea kwa COVID-19 kwa wapendwa nje ya nyumba yako. Mawazo mengine yanajumuisha:



## Kupanga mkutano wako:

- Acha iwe ndogo Punguza idadi ya wageni, na uhimize ushiriki kupitia mtandao.
- Hakikisha watu ambao ni wagonjwa, watu ambao wamejitenga kwa sababu wamepatikana kuwa na maambukizi, watu walio katika karantini, au watu ambao wanasubiri matokeo ya kipimo hawahudhuri.
- Waombe wageni kuvaa barakoa wakati hawawezi kudumisha umbali kati yao na wengine, hasa wanapokuwa ndani ya nyumba.
- Andaa mipangilio ya kuketi ili kuruhusu umbali unaofaa kati ya watu ikiwezekana, fikiria kila familia kuketi kwenye meza tofauti.
- Panga mkusanyiko mfupi.
- Dumisha orodha ya wageni na habari ya mawasiliano iwapo mtu yeyote atahitaji kujulishwa kuhusu mfiduo wa kesi chanya ndani ya kikundi chako.



## Kwenye mkusanyiko wako:

- Waombe wageni wadumisha umbali kati yao na wavae barakoa.
- Kusanyikeni nje, ikiwezekana.
- Boresha uingizaji hewa mkiwa ndani ya nyumba, hasa wakati wa kula (kufungua madirisha, washa kiyoyozi, n.k.).
- Osha mikono kwa ukawaida, na uepuka kugusa sehemu nyingi.
- Uwe na vieuzi vingi kwa ajili ya wageni wako.



## Wakati wa kuandaa / kupakua chakula:

- Kila mtu anayehusika katika utayarishaji wa chakula anapaswa kuvaa barakoa.
- Punguza idadi ya watu walio katika eneo la utayarishaji wa chakula.
- Epuka mtindo wa wageni kuleta chakula walichoandaa nyumbani mwao.
- Fikiria kuwa na mtu mmoja anayepakua chakula chote, badala ya watu binafsi kujipakulia.
- Jaribu kutumia vyombo vinavyoweza kutupwa baada ya matumizi.



## Baada ya mkusanyiko wako:

- Mtu yeyote atakayeugua anapaswa kujitenga na kupimwa.
- Ikiwa mgeni yeyote atapatikana na ugonjwa, wageni wote wanapaswa kujulishwa kwamba wanapaswa kukarantini, wachunguze dalili, na wapimwe ikiwa watapata dalili.